



Matayarisho fedha na bajeti ya serikali ya Kaunti, Oktoba 2016

Utangulizi

Kila wananchi ana jukumu ya kuhusika na matayarisho ya bajeti za serikali ya Kaunti yake. Wananchi wote wana haki ya kujua jinsi serikali inavyotumia fedha zetu. Kusababu fedha za umma ni fedha ya raia wote zimetokana na ushuru wanaolipa wananchi wa Kenya kama vile ushuru wa mapato, VAT na ushuru wa mauzo na bidhaa zinginezo tunazonunua kila siku. Fedha za umma pia zinajumuisha mikopo na misaada inayopokelewa na serikali kwa niaba ya mwananchi. **Serikali haina fedha zake binafsi, fedha zote ni za raia wa Kenya na husimamiwa na serikali kwa niaba wananchi.**

Katiba ya mwaka 2010 imeleta sheria mpya inayoshinikiza usawa katika ugavi wa rasilimali utakaofaidi wakenya wote. Sheria hizi mpya zimetengenezwa kuzuia ubadhirifu na kuadhibu wanaofuja rasilimali za umma. Sheria ya usimamizi wa fedha (PFM) imetoa sheria zinazoelekeza jinsi serikali ya kitaifa na serikali za kaunti zinaweza kupata fedha na mikakati ya kuzitumia. Sheria ya fedha za umma pamoja na katiba ya mwaka 2010, ndiyo kielelezo kikuu kinachomwelekeza rais, wabunge, magavana, maseneta na wawakilishi wa kaunti, na mwananchi wa kawaida kuhusu majukumu yao katika maamuzi ya jinsi fedha za umma zinapaswa kutumiwa. Ikiwa unajali jinsi serikali inavyotumia fedha zako, na jinsi unavyoweza kushinikiza mkondo huo, basi itakuwa muhimu pia kufahamu sheria ya kusimamia fedha za umma.

Ratiba ya bajeti.

Augosti 30. Hazina ya kitaifa hutoa taarifa kwa mashirika ya kiserikali na kuanzisha harakati

ya bajeti na kushirikisha umma kwa kufuata muongozo maalum. Afisa mkuu wa fedha katika kaunti lazima pia asambaze taarifa kufikia tarehe hii vilevile katika kaunti.

Septemba 1. Kaunti lazima watayarishwe na kuwasilisha taarifa ya mipangilio ya miradi ya maendeleo katika bunge la serikali ya kaunti kufikia tarehe hii. Mpangilio huo husambazwa kwa umma katika siku 7.

Septemba 1 hadi Februari 15. Wakati huu hazina ya kitaifa na baadhi ya wizara na mashirika ya serikali hujadiliana na umma na wadau. Aidha vikao pia vya umma huandaliwa na maoni yao kujumuishwa katika mapendekezo ya bajeti.

Novemba. Serikali lazima ichapishe mtazamo wa bajeti ili ikaguliwe na kutofautisha utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita na mitzamo wa bajeti kutoka kwa taarifa ya sera za bajeti mwezi Februari. Hata hivyo mtazamo wa bajeti ya kaunti hauna tarehe ya mwisho kuwasilishwa katika bunge la kaunti lakini itayarishwe katika wakati huu.

Desemba 15. Serikali inapaswa kuchapisha ripoti na kutekelezwa katika miezi mitatu ya kwanza katika mwaka wa kifedha kuanzia Julai hadi Septemba kabla siku 45 baada ya robo ya kwanza ya mwaka wa kifedha kuisha.

January 1. Kufikia mwezi Januari kila mwaka tume ya mgao wa mapato ya kitaifa CRA hutoa mapendekezo yake kwa serikali ya kaunti na ya kitaifa.

Februari 15. Waziri wa fedha hutoa taarifa ya sera ya bajeti wakati huu. Kadhalika ndiyo tarehe ya mwisho ya kuwasilisha taarifa ya mikakati ya kudhibiti mikopo na mswada wa mgao wa mapato kwa serikali ya kaunti bungeni.

Februari 28. Tarehe ya mwisho ya kuidhinisha taarifa ya sera za bajeti bungeni. Hii ndiyo tarehe ya mwisho pia ya kuwasilisha taarifa kuhusu mikakati ya kifedha katika serikali za kaunti.

Machi 1. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha taarifa ya sera za bajeti kwa umma.

Machi 16. Hii ndiyo tarehe ya mwisho ya kupitisha mswada wa mgao wa mapato ya kitaifa katika kaunti.

Aprili 30. Hii ndiyo tarehe ya mwisho kwa waziri wa fedha kuwasilisha makadirio ya bajeti bungeni. Ni tarehe ya mwisho pia kwa idara ya mahakama na tume ya huduma za bunge kutoa bajeti yao pia bungeni. Mapendekezo ya bajeti ya kaunti pia huwasilishwa wakati huu

Mei. Huu ndio wakati kamati ya bunge kuhusu fedha na bajeti hufanya vikao vya umma kukusanya maoni.

Juni. Mswada wa kitaifa wa fedha unaoidhinisha kukusanya ushuru huwasilishwa bungeni. Mswada wa fedha wa kaunti pia huwasilishwa katika bunge la kaunti.

Juni 30. Huu ndiyo mwisho wa mwaka wa kifedha kwa mswada wa matumizi ya fedha kupitishwa na bunge ili kuidhinisha matumizi ya fedha za bajeti ya mwaka mpya.

Julai. Katika mwezi huu makadirio ya bajeti yaliopitishwa husambazwa kwa umma.

ⁱ Toleo hili limefanikishwa kwa ungozi ya karatasi la Shirika ya Kimataifa la Bajeti (International Budget Partnership - IBP).